# Ulumbi wa Ipara

## na Hadithi Nyingine





Fred C. N. W. Simiyu
na
Emmanuel Masaka

# Ulumbi wa Ipara

## na Hadithi Nyingine

Kimetolewa kwa Ken Walibora Corner – Kibabii University Library na Waandishi.

19/11/2025

Fred, C. N. W. Simiyu

na

Emmanuel Masaka

**© Fred C. N. W. Simiyu na Emmanuel Masaka, 2025**

**ISBN: 978-9966-59-033-6**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa njia yoyote ile bila idhini ya waandishi.

Kimechapishwa na
Chuo Kikuu cha Kibabii
S.L.P. 1699-50200
Bungoma, Kenya.

# Maelezo Kuhusu Waandishi

**Aaron Kibet Chenibei** ni mwalifunzi wa mwaka wa pili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Anasomea Taaluma ya Elimu katika masomo ya Jiografia na Kiswahili. Ni mzaliwa wa Gatuzi la Bungoma. Ni mwandishi chipukizi katika kazi za fasihi zikiwemo hadithi fupi na ushairi. Ana ari ya kuibuka kuwa mwandishi mahiri katika siku za usoni.

**Andrew Watuha** ni mtaalamu mahiri wa elimu na mwenye tajiriba ya zaidi ya miaka 36 katika sekta ya elimu. Amechangia katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili na vyuo vikuu nchini Kenya. Utaalamu wake unahusisha uratibu wa mitaala, uundaji wa mikakati ya ufundishaji, na usimamizi wa programu za walimu. Isitoshe, ni mwandishi aliyechangia pakubwa katika uandishi wa vitabu 36 vya kiada vya shule za msingi na upili maarufu kama *Kiswahili Kitukuzwe* pamoja na vitabu vingine vya hadithi vilivyochapishwa na shirika la KLB. Pia, ameshiriki katika uhariri wa *Kamusi Teule ya Kiswahili*. Kwa sasa, anafundisha Isimu katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Ni mtafiti wa Kiswahili anayehudhuria na kushiriki kwa dhati katika makongamano ya Kiswahili. Yey pia ni mkalimani na mtafsiri stadi. Vilevile, ni mshauri wa somo la Kiswahili katika Baraza la Mitihani (*KNEC*) nchini Kenya. Isitoshe, amechangia kwa kiasi kikubwa katika michezo kama mwamuzi na kocha wa kimataifa wa mchezo wa Mpira wa Mikono.

**Emmanuel Masaka** ni mzaliwa wa Kaunti ya Busia, Eneo Bunge la Butula. Akiandika hadithi hii, alikuwa mwanachuo katika Chuo Kikuu cha Kibabii mwaka wa nne. Emmanuel Masaka alimaarufu *Masaka Mkuu* ni mwandishi wa hadithi fupi, tamthilia na mashairi.

Alishiriki katika kuandika diwani ya hadithi fupi ya: *Barua ya Hukumu na Hadithi Nyingine*. Aidha, alishiriki katika kuandika wasifu wa *Timothy Omusikoyo* (Shujaa wangu). Masaka Mkuu amehudumu kama Mhariri Mkuu wa Chama cha Kiswahili cha Kibabii (CHAKIKI) kwa mihula miwili mtawalia. Alisomea Taaluma ya Elimu, tahasusi ya Kiswahili na Jiografia.

**Fred Cheloti Nalyanya Wanjala Simiyu** ni msomi, mwalimu na mwandishi wa Fasihi, Tafsiri, Utamaduni na Lugha ya Kiswahili mwenye tajriba pana. Ana shahada ya Uzamifu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika kutoka Ndaki ya Kenyatta. Aidha, yeye ndiye mwandishi wa *Kitovu cha Fasihi Simulizi; Misingi ya Ukalimani na Tafsiri; Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili; Concice Trilingual English-Kiswahili-French Dictionary; Safina ya Utafiti wa Fasihi Simulizi; na Kiswahili na Uchumi wa Kidijitali*. Ameandika na kuchapisha makala zaidi ya ishirini katika majarida tajika. Kwa sasa, yeye ni Mwenyekiti wa CHAKITA na Mhadhiri Mwandamizi wa Taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma - Kenya.

**Fred Wanjala Wanyonyi** ni mzamifu katika Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kibabii. Alizaliwa katika kijiji cha Ngwelo, Gatuzi la Bungoma. Fred alisomea shule ya msingi ya *Misikhu R.C Boys* kisha akajiunga na shule ya upili ya kitaifa ya *Friends School Kamusinga*. Alipata shahada yake ya kwanza kutoka Chuo Kikuu cha Moi ambapo alifuzu kama mwalimu wa Somo la Kiswahili na Dini. Alihitimu Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Fred ameandika na kuchapisha makala kama vile *Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya* na *Methangano ya Babukusu kama Nguzo Kuu ya Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa Kazi Teule za Ken Walibora.*

Aidha, yeye ndiye mwandishi wa hadithi fupi ya *Friday Night* na *Am Not Satisfied*.

**Henry Indindi** (***Mjileo wa Indindi***) - ni mtaalamu farisi wa Kiswahili, anayetambulika na kuheshimika kwa fikra zake za kimkakati katika kufanikisha ubora wa Kiswahili. Ana tajriba ya zaidi ya miaka 23 katika sekta za Elimu na Mawasiliano. Amefundisha katika shule za upili na vyuo vikuu, kufanya kazi katika mashirika ya uchapishaji, pamoja na kuandika zaidi ya vitabu 20. Ana ghera kubwa katika masuala ya Tafsiri na Ukalimani, Uhariri na Usomaji wa Kisarifu na Utafiti. Hali kadhalika, yeye hufanya kazi ya Uhazili katika makongamano ya kimataifa. Vilevile, amechangia maneno na kuhariri kamusi kadhaa za Kiswahili kama vile *Kamusi Pevu ya Kiswahili*, *Kamusi Teule ya Kiswahili* na *Kamusi Elezi*. Mara kwa mara, yeye hushiriki kwenye vipindi vya runinga na redio nchini Kenya na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa katika programu za kielimu na uchambuzi wa siasa, diplomasia na uongozi (*KBC Channel 1*, *KBC* Idhaa ya Taifa, *TV47*, Radio 47, Radio Maisha, Ingo FM, Azam TV na U-FM, Dar es Salaam) pamoja na magazeti ya Kiswahili, mathalan *Taifa Leo*. Yeye hushiriki na kuchangia kikamilifu katika makongamano ya Kiswahili na ya kitaaluma; kitaifa na kimataifa. Kwa sasa, ni Mkurugenzi Mkuu Mtendaji katika kampuni ya *Mjileo Communications Ltd*.

**Hillary Mauka Mukoya** ni mzawa wa Gatuzi la Bungoma aliyezaliwa mnamo 15/07/1987, Njoro, Gatuzi la Nakuru nchini Kenya. Ana shahada ya *B.Ed (Arts)* kutoka Chuo Kikuu cha Moi. Mwaka 2019 alifuzu na Shahada ya Uzamili katika Elimu ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii. Kwa sasa anaendeleza masomo ya uzamifu katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Amefundisha katika shule kadhaa za sekondari. Hivi sasa anafundisha katika Shule ya Upili ya Wasichana ya Askofu Sulumeti-Chelelemuk. Pia, ni Mtahini wa karatasi ya pili

ya Kiswahili (102/2) nchini Kenya. Vilevile, amekuwa mhadhiri wa muda katika Ndaki ya Kibabii na Ndaki ya *Management University of Africa* (MUA). Aidha, ni mwandishi wa hadithi fupi ya *Moja Kwisha* katika diwani ya *Wino Usiofutika na Hadithi Nyingine*.

**Joyce Nechesa Burudi** ni mwalimu mahiri wa Kiswahili mwenye tajiriba. Ana Shahada ya Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na Uzamili kutoka ***MMUST.*** Kwa sasa, anendelea na Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Ni mwandishi mwenza wa *Upeo wa Sarufi, Mwongozo wa Damu Nyeusi na Hadithi nyingine, Mwongozo wa Kigogo, Mkusanyiko wa Mswali na Majibu ya Kigogo na Tumbo Lisilishiba na Hadithi Nyingine.*

**Juliet Burudi** ni mwanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii, mwaka wa tatu. Ana hamu kuu kuchangia katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kupitia utafiti na uandishi.

**Kelvin Ekirapa Okitoi** ni mwalimu wa Kiswahili na Historia. Ni mwandishi wa riwaya, tamthilia, mashairi na hadithi fupi. Alisomea shahada ya ualimu katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Alichangia pakubwa katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili katika runinga ya *K.B.C* katika kipindi *Tamrini* kitengo cha sanaa ya uandishi mwaka 2023. Sasa hivi, anafundisha katika Shule ya Upili ya Aboloi Kaunti ya Busia, Kata Ndogo ya Teso Kaskazini. Mbali na kuwa mwandishi chipukizi, alihudumu kama Naibu Mwenyekiti wa Chama cha Kiswahili cha Kibabii (CHAKIKI). Pia, ameigiza filamu mbalimbali kama vile: *Mkosoaji, Pain of Pendo, The Soul at Risk* na *Lust for Love,* yote katika lugha ashirafu ya Kiswahili.

**Lutta John Makomere** ni mwalifunzi katika Chuo Kikuu cha Kibabii anayesomea Shahada ya kwanza katika somo la Kiswahili na Jiografia. Yeye ni mwandishi wa Riwaya, mashairi na pia hadithi

fupi. Mbali na hayo, yeye ni Katibu Mratibu wa Chama cha Kiswahili Kibabii (2024/25).

**Moses Omoit** ni mzaliwa wa eneo la Ang'urai Gatuzi la Busia. Ni mwalifunzi wa mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Moses pia ni mwenyekiti wa Chama cha Kiswahili cha Kibabii – CHAKIKI.

**Mwalimu Jackson Ngati** ni mwanachuo katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Pia, yeye ni mwandishi wa riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Tayari amechapisha riwaya ya *Machozi ya Gizani* na kazi nyinginezo za kifasihi.

**Nester Ateya** ni mwalimu mwenye tajriba pana katika ufundishaji na utahini wa lugha na fasihi nchini Kenya, Ni mwandishi na mtafiti wa taaluma ya Isimu. Ana shahada ya *Bed Arts* katika Kiswahili na Hstory kutoka Chuo Kikuu cha Moi; shahada ya Uzamili katika Elimu ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii. Kwa sasa, anasomea shahada ya Uzamifu katika Taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii.

**Noah Munda Majele** ni Mhadhiri Msaidizi na mzamifu katika Taaluma ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kibabii. Ni mzaliwa wa Mtaa wa Taru, Kaunti Ndogo ya Samburu, Kaunti ya Kwale. Kwa sasa, anafundisha katika Shule ya Upili ya Wasichana ya Mackinnon. Ana shahada ya kwanza ya Ualimu katika Kiswahili na somo la Dini kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii. Vilevile, ana shahada ya Uzamili katika Elimu ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii. Ameandika na kuchapisha makala mbalimbali yakiwa ni pamoja na: *Mchango wa Mofofonolojia ya Kiduruma kwa Ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili, Responsive Use of Artificial Intelligence in Kiswahili Language Learning to University Students in Kenya,* na *Nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika Mawasiliano ya Vijana Wakati wa*

*Harakati za Kupinga Mswada wa Fedha wa Mwaka 2024.*

**Oscar Segero Kiboi** ni mwanachuo wa Chuo Kikuu cha Kibabii. Ni mzaliwa wa Magharibi mwa Kenya katika Gatuzi la Bungoma. Ni malenga pamoja na mwandishi wa hadhithi fupi. Ameshiriki katika uandishi wa *Diwani ya Halua ya Ushairi*. Anasomea Shahada ya Ualimu katika somo la Kiswahili na Jiografia. Aidha, yeye ni mtafiti katika safu nzima ya Fasihi.

**Priscilla Nekesa** ni mzaliwa na Gatuzi la Vihiga - Kenya. Ni mwalimu wa Kiswahili na mwandishi chipukizi aliye na azma ya kuwa mwandishi tajika na mahiri katika kazi za kifasihi haswa fasihi simulizi. Alifuzu kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii, Novemba 2024. Ana Shahada ya Ualimu (Kiswahili na Historia). Aliwahi kuhudumu katika Chama cha Kiswahili cha Kibabii (CHAKIKI) kama Mhazini na baadaye kama Mwenyekiti.

**Rehema Muhammed** ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kibabii anayesomea Taaluma ya Elimu, somo la Kiswahili na Jiografia. Akiandika hadithi hii alikuwa mwaka wa tatu, mwaka wa masomo wa 2024/25.

# Yaliyomo

Maelezo Kuhusu Waandishi .................................................... iii

Utangulizi .................................................................................... xi

Ulumbi wa Ipara
*Noah Munda Majele & Fred, C. N. W. Simiyu* .............................. *1*

Bara la Ipara
*Fred Wanjala Wanyonyi* ........................................................ *21*

Profesa wa Kiswahili
*Hillary Mauka Mukoya* .......................................................... *29*

Moyo wa Dhahabu
*Kelvin Ekirapa* ....................................................................... *41*

Mwamba Imara
*Priscilla Nekesa* ..................................................................... *49*

Nakuenzi Profesa
*Emmanuel Masaka* .................................................................. *57*

Chanda Chema
*Aaron Kibet Chenibei* ............................................................. *65*

Sitajuta Kumjua
*Moses Omoit* .......................................................................... *73*

Ametoka Vitabuni
*Mwalimu Jackson Ngati* .......................................................... *79*

Ila kwangu Tofauti
*Rehema Muhammed* ................................................................ *87*

Bingwa wa Elimu
*Juliet Burudi* ........................................................................... *95*

Sauti ya Ulimwengu
*Kiboi Oscar Segero* .................... *101*

Gwiji Mahiri
*Lutta John Makomere*.................... *105*

Nyayo za Nguli wa Taaluma
*Watuha Andrew & Indindi Henry*.................... *113*

Profesa Mwenye Kofia Nyingi
*Joyce Burudi*.................... *119*

Kivuli
*Ateya Nester* .................... *131*

# Ulumbi wa Ipara

## na Hadithi Nyingine









"Uyakinifu ni ithibati ya matukio hayo ya kihistoria kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi. Ubunifu ni ufundi na upekee maalum wa mtunzi wa fasihi anaotumia kueleza matukio ya kihistoria. *Diwani ya Ulumbi wa Ipara na Hadithi Nyingine* imejengwa katika ithibati ya matukio ya kihistoria yaliyowasilishwa kiubunifu. ……. Kwa hivyo, wasifu na otografia hurejelea uyakinifu wa kihistoria kuhusu maisha halisi ya watu kwa njia ya kibunifu…….. Waandishi wa *Diwani ya Ulumbi wa Ipara na Hadithi Nyingine* wametoa mchango wao mdogo. Nawatakia usomaji mwema."

**Dkt. Fred, C. N. W. Simiyu,**
**Tarehe 23/07/2025,**
**Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya.**

ISBN 978-9966-59-033-6

9 789966 590336

Kimechapishwa na
Kibabii University Press
S.L.P. 1699-50200
Bungoma, Kenya.